اللغة السواحيلية

# Misingi mitatu na ahidi wake




Mtunzi

Sheikhul Islami

**Muhammad bin Abdul wahhab**

1115 - 1206



Islamhouse.com

المحتوى الإسلامي


ثلاثة الأصول وأدلّها

# Misingi mitatu na ahidi wake

: Mtunzi: Sheikhul Islami Muhammad bin Abdul wahhab.

شركاء التنفيذ:

دار الإسلام
جمعية الربوة
رواد الترجمة
المحتوى الإسلامي

يتاح طباعة هذا الإصدار ونشره بأي وسيلة مع الالتزام بالإشارة إلى المصدر وعدم التغيير في النص.

Telephone: +966114454900
ceo@rabwah.sa
P.O.BOX: 29465
RIYADH: 11557
www.islamhouse.com

# Utangulizi wa msambazaji:

Kwa jina la Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehema Mwenye kurehemu.

Kila sifa njema zinamstahiki Mwenyezi Mungu bwana wa walimwengu, na Rehema na Amani ziwe juu ya Nabii Muhammad na familia yake na wanafunzi wake na yeyote aliyeongoka kwa uongofu wake mpaka siku ya mwisho. Ama baada ya hayo:-

Hakika katika mambo anayotakiwa kuyatilia umuhimu muislamu, na mambo makubwa anayotakiwa kuyapupia, ni yale yanayohusiana na itikadi, na misingi ya ibada, kwani kuwa na itikadi salama na kufuata mafundisho ya Mtume, mambo haya yana nafasi kubwa katika kukubaliwa matendo pamoja na manufaa yake kwa mja.

Na ameuneemesha Mwenyezi Mungu umma huu, na akaukirimu kwa kuufanyia wepesi wa kupatikana wanachuoni walioongoka, na taa zing'aazo, walio angaza njia, na wakabainisha ya wajibu na

yale yasiyotakiwa, na yenye kudhuru na yenye kunufaisha, katika mambo nyeti na mambo matukufu, basi Mwenyezi Mungu awalipe kheri kwa niaba ya uislamu na waislamu malipo mema.

Na miongoni mwa wakubwa katika maimamu hao, na maarufu zaidi ni sheikhul Islam na kiigizo cha umma Imamu Muhammad bin Abdul Wahhab Mwenyezi Mungu amjaze malipo mengi na thawabu nyingi na amuingize peponi bila hesabu, kwani amejitahidi Mwenyezi Mungu amrehemu katika kuibainisha haki kwa ushahidi, na akapambana juu ya hilo kwa moyo wake na ulimi wake na umri wake, mpaka Mwenyezi Mungu akaziokoa kupitia yeye umma mbali mbali kutoka katika giza la ukafiri na ujinga kuja katika nuru ya elimu na imani.

Na kitabu hiki kilichoko mikononi mwetu kimekusanya jumbe tatu za imamu huyu, nazo ni (Misingi mitatu na ushahidi wake, na sharti za swala na wajibu wake na nguzo zake, na kanuni nne).

Na Jumbe hizi ni katika Jumbe zake muhimu sana na zilizokamilika katika kubainisha misingi ya itikadi na ibada, amekusanya Mwenyezi Mungu amrehemu yaliyowajibu kwa kila muislamu kuyafahamu na kuyafanyia kazi katika mambo ya msingi katika dini yake.

Pamoja na kumtahadharisha muislamu kutokana na utata (shub-ha) za walinganiaji wa kishirikina ambao wanawatia shaka watu kwa madai yao kuwa wao wanaishia katika shirki yao katika kumshirikisha Mwenyezi Mungu katika uungu pekee, akabainisha kosa lao na

akajibu utata wao kutoka katika kitabu cha Mwenyezi Mungu na Sunna za Mtume wake- Rehema na Amani ziwe juu yake.

Amekitunga kitabu hiki -Mwenyezi Mungu amrehemu- kwa ajili ya wanaoanza kujifunza, na akajitahidi kukirahisisha na kukifupisha, mpaka kikatoka katika muonekano mzuri na faida kubwa, hata mtoto mdogo anaweza kukielewa lakini pia hata mtu mzima naye anakihitajia, hivyo manufaa yake yakawa makubwa, na kheri

zake zikawa nyingi; kwa ukubwa wa kiwango cha maudhui zake na utukufu wa mada zake.

Bila shaka Wizara inayohusika na mambo ya kiislamu na Wakfu na Da'awa na utoaji wa muongozo, imetilia umuhimu katika kuweka wasimamizi katika machapisho na kuyasambaza, pale ilipoona katika risala hizi kuna faida kubwa zilizofichikana, tena mfumo wake ni mwepesi na rahisi, pamoja na utukufu wa kiwango cha maudhui zake na umuhimu wake; ikaona kuwa katika mambo ya msingi zaidi ya kutiliwa umuhimu na kusambazwa, ni kuwalingania watu kuja kwa Mwenyezi Mungu kuliko sawa kwa hekima na njia iliyosalama, na kuwanasihi kwa ajili ya Mwenyezi Mungu na Mtume wake na kitabu chake na

Dr. Abdallah Bin Ahmad Al Zaid

# Mambo ya wajibu kwa muislamu kujifunza:

Kwa jina la Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehema Mwenye kurehemu.

Tambua akurehemu Mwenyezi Mungu, yakwamba ni wajibu kwetu kujifunza mambo manne.

(La kwanza) Ni Elimu: Nayo ni kumfahamu Mwenyezi Mungu, Na kumfahamu Nabii wake, na kuifahamu dini ya uislamu kwa ushahidi.

(La pili) kuifanyia kazi.

(La tatu) kuifikisha. (La nne) kuvumilia juu ya maudhi yapatikanayo kwenye kulingania, na ushahidi ni kauli yake Mtukufu: Kwa jina la Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema mwenye kurehemu. "Naapa kwa wakati wa Laasiri" "Kuwa Binadamu yupo katika

Hasara". "Isipokuwa wale waliomuamini Mwenyezi Mungu, na wakafanya amali njema, na wakausiana wao kwa wao kushikamana na haki, na wakausiana kusubiri"[1].

[1] . Suratul Al A'sri: 1-3.

Na amesema Imamu Shafy, Allah amrehemu: Laiti asingeteremsha Mwenyezi Mungu hoja yoyote juu ya viumbe wake isipokuwa sura hii basi ingeliwatosha.

Na amesema Bukhari Mwenyezi Mungu Mtukufu amrehemu katika (Juzuu ya 1 uk 45)

(Mlango wa) Elimu kabla ya kauli na matendo, na ushahidi ni kauli yake Mtukufu: "Tambua hakika kuwa hapana Mola apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Mwenyezi Mungu na uombe msamaha kwa

dhambi zako"[2]. Hivyo Basi akaanza na elimu kabla ya kauli na matendo".

(Tambua) Akuhurumie Mwenyezi Mungu, yakwamba ni lazima kwa muislamu wa

kiume na wa kike kujifunza mambo haya matatu na kuyafanyia kazi.

(La kwanza) Nikuwa Mwenyezi Mungu ametuumba na akaturuzuku na wala hakutuacha hivi bure, bali akatutumia kwetu sisi Mtume, Ili atakayemtii aingie peponi na atakaye muasi aingie motoni, na ushahidi ni kauli yakeMwenyezi Mungu Mtukufu: "Hakika sisi tumetuma kwenu nyinyi, watu wa Makkah, Muhammad kuwa ni

---

[2] . Suratu Muhammad: Aya ya: 19.

Mtume, mwenye kutoa ushahidi wa ukafiri na uasi unaotokana na nyinyi, kama vile tulivyomtuma Mūsā kuwa ni Mtume kwenda kwa Fir’aun "

﴿إِنَّآ أَرۡسَلۡنَآ إِلَيۡكُمۡ رَسُولٗا شَٰهِدًا عَلَيۡكُمۡ كَمَآ أَرۡسَلۡنَآ إِلَىٰ فِرۡعَوۡنَ رَسُولٗا ١٥ فَعَصَىٰ فِرۡعَوۡنُ ٱلرَّسُولَ فَأَخَذۡنَٰهُ أَخۡذٗا وَبِيلٗا ١٦﴾ [المزمل: 15-16].[3]

. "Lakini Firauni alimuasi huyo Mtume, basi tukamshika mshiko wa mateso"[4]Suratul Muzzammil: Aya: 15, 16.

(La pili): Nikuwa Mwenyezi Mungu haridhii kushirikishwa pamoja naye katika ibada zake yeyote, si Malaika aliyekaribu wala Nabii aliyetumwa, na ushahidi ni kauli yake Mtukufu:

﴿وَأَنَّ ٱلۡمَسَٰجِدَ لِلَّهِ فَلَا تَدۡعُواْ مَعَ ٱللَّهِ أَحَدٗا ١٨﴾[الجن: 18][5]

"Na kwa hakika misikiti yote ni ya Mwenyezi Mungu peke yake, basi msiabudu humo yeyote asiyekuwa Yeye". Suratul Jinn, Aya: 18.

(La tatu): Nikuwa mwenye kumtii Mtume na akampwekesha Mwenyezi Mungu, haitakiwi kwake kumpenda mwenye kumpiga vita Mwenyezi Mungu na

---

[3] ৩] সূরা আল-মুযযাম্মিলের দু'টি আয়াত: ১৫-১৬।

[4] Suratul Muzzammil: Aya 15-16.

[5] ৪] সূরা আল-জিন: আয়াত:১৮।

Mtume wake hata kama atakuwa ndugu wa karibu, na ushahidi ni kauli yake Mtukufu:

﴿لَّا تَجِدُ قَوۡمٗا يُؤۡمِنُونَ بِٱللَّهِ وَٱلۡيَوۡمِ ٱلۡأٓخِرِ يُوَآدُّونَ مَنۡ حَآدَّ ٱللَّهَ وَرَسُولَهُۥ وَلَوۡ كَانُوٓاْ ءَابَآءَهُمۡ أَوۡ أَبۡنَآءَهُمۡ أَوۡ إِخۡوَٰنَهُمۡ أَوۡ عَشِيرَتَهُمۡۚ أُوْلَٰٓئِكَ كَتَبَ فِي قُلُوبِهِمُ ٱلۡإِيمَٰنَ وَأَيَّدَهُم بِرُوحٖ مِّنۡهُۖ وَيُدۡخِلُهُمۡ جَنَّٰتٖ تَجۡرِي مِن تَحۡتِهَا ٱلۡأَنۡهَٰرُ خَٰلِدِينَ فِيهَاۚ رَضِيَ ٱللَّهُ عَنۡهُمۡ وَرَضُواْ عَنۡهُۚ أُوْلَٰٓئِكَ حِزۡبُ ٱللَّهِۚ أَلَآ إِنَّ حِزۡبَ ٱللَّهِ هُمُ ٱلۡمُفۡلِحُونَ٢٢﴾[المجادلة: 22].[6]

"Hutakuta, ewe Mtume, watu wanaomuamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho na wanaofanya matendo waliyoamrishwa na Mwenyezi Mungu, wakiwapenda na kuwategemea wale wanaomfanyia uadui Mwenyezi Mungu na Mtume wake na wanaoenda kinyume na amri zao,hatakama itakuwa ni baba zao au

watoto wao au ndugu zao au jamaa zao wa karibu. Hao wanaofunga urafiki kwa ajili ya Mwenyezi Mungu na wanaosimamisha uadui kwa ajili yake ndio wale ambao Mwenyezi Mungu Ameithibitisha Imani ndani ya nyoyo zao na Akawatia nguvu kwa

kuwapa ushindi utokao kwake na msaada dhidi ya adui yao duniani, na Atawaingiza huko Akhera kwenye mabustani ya Peponi ambayo chini ya miti yake inapita mito, hali ya kukaa humo milele, Amewapa radhi zake na

[6] ৫] সূরা আল-মুজাদালাহ: আয়াত: ২২।

hatawakasirikia na wao wameridhika na Mola wao kwa yale aliyowapatia ya utukufu na daraja kubwa. Hilo ndiyo kundi la Mwenyezi Mungu,eleweni vywema kuwa kundi la Mwenyezi Mungu ndilo lenyekufaulu". Al Mujadala: 221 .

## Utakasifu ambao ni mila ya Ibrahim ndiyo Ibada ya kumuabudu Mwenyezi Mungu peke yake.

Tambua, akuongoze Mwenyezi Mungu katika utiifu wake: Yakuwa utakasifu ndiyo mila ya Ibrahim: Nao ni kumuabudu Mwenyezi Mungu, yeye pekee kwa kumtakasia dini, na kwa hilo amewaamrisha Mwenyezi Mungu viumbe wote, na akawaumba kwa ajili hiyo, kama alivyosema Mwenyezi Mungu Mtukufu: {Sikuwaumba majini wala watu ila ni kwa lengo la

kuniabudu}[7]Na maana ya: Waniabudu: yaani: wanipwekeshe.

Na kubwa aliloliamrisha Mwenyezi Mungu ni tauhidi, nayo ni kumpwekesha Mwenyezi Mungu kwa Ibada.

Na kubwa alilolikataza Mwenyezi Mungu ni Shirki: Nayo ni kumuomba asiyekuwa yeye pamoja naye, na ushahidi ni kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu: "Na muabuduni Mwenyezi Mungu na wala msimshirikishe yeye na chochote"[8].

---

[7] . Dhariyat: 56.
[8] . Al Nisaa: Aya ya: 36

(Utakapoambiwa): Ni ipi misingi mitatu ambayo ni wajibu kwa Mwanadamu kuifahamu?

Basi sema: Ni mja kumjua Mola wake, na Dini yake na Nabii wake Muhammadi- Rehema na Amani ziwe juu yake.

Utakapo ulizwa: Nani Mola wako?

Basi sema: Mola wangu ni Allah aliyenilea na akawalea walimwengu wote kwa neema

zake, na ndiye muabudiwa wangu sina mimi muadiwa mwingine zaidi yake, na ushahidi ni kauli yakeMwenyezi Mungu Mtukufu: "Shukurani zote njema anastahiki Mola wa viumbe vyote"[9]Na kila kisichokuwa Mwenyezi Mungu hicho ni Kilimwengu, na mimi ni mmoja miongoni mwa walimwengu.

Utakapo ulizwa: ni kwa kitu gani umemjua Mola wako mlezi?

Basi sema: Nimemjua kwa alama zake na viumbe vyake, na miongoni mwa alama zake ni usiku na mchana na jua na mwezi, na miongoni mwa viumbe vyake ni mbingu Saba na Ardhi Saba na vyote vilivyomo na vilivyo kati yake, na ushahidi ni kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu:

---

[9] Suratul Faatiha Aya: 2.

﴿وَمِنۡ ءَايَٰتِهِ ٱلَّيۡلُ وَٱلنَّهَارُ وَٱلشَّمۡسُ وَٱلۡقَمَرُۚ لَا تَسۡجُدُواْ لِلشَّمۡسِ وَلَا لِلۡقَمَرِ وَٱسۡجُدُواْۤ لِلَّهِ ٱلَّذِي خَلَقَهُنَّ إِن كُنتُمۡ إِيَّاهُ تَعۡبُدُونَ ۝٣٧﴾ [فصلت: 37].[10]

"Na miongoni mwa hoja za Mwenyezi Mungu kwa viumbe vyake, dalili za upweke

wake na ukamilifu wa uweza wake, ni kutofautiana mchana na usiku na kufuatana (kila mojawapo kuufuata mwingine) na kutofautiana jua na mwezi na kufuatana, vyote hivyo viko chini ya uendeshaji wake. Msilisujudie Jua wala Mwezi, kwani hivyo viwili vinaendeshwa na vimeumbwa; na msujudieni Mwenyezi Mungu Aliyeviumba, iwapo nyinyi kwa kweli mnafuata amri yake, mnasikia na mnamtii yeye, basi muabuduni yeye peke yake asiye na mshirika". Suratu Fusswilat: 37.

Na kauli yake Mtukufu:

﴿إِنَّ رَبَّكُمُ ٱللَّهُ ٱلَّذِي خَلَقَ ٱلسَّمَٰوَٰتِ وَٱلۡأَرۡضَ فِي سِتَّةِ أَيَّامٖ ثُمَّ ٱسۡتَوَىٰ عَلَى ٱلۡعَرۡشِۖ يُغۡشِي ٱلَّيۡلَ ٱلنَّهَارَ يَطۡلُبُهُۥ حَثِيثٗا وَٱلشَّمۡسَ وَٱلۡقَمَرَ وَٱلنُّجُومَ مُسَخَّرَٰتِۭ بِأَمۡرِهِۦٓۗ أَلَا لَهُ ٱلۡخَلۡقُ وَٱلۡأَمۡرُۗ تَبَارَكَ ٱللَّهُ رَبُّ ٱلۡعَٰلَمِينَ ۝٥٤﴾[الأعراف: 54][11]

"Hakika Mola wenu ni Mwenyezi Mungu aliyeziumba Mbingu na Ardhi kwa siku sita. kisha akatulizana juu ya

---

[10] ৯] সূরা ফুসসিলাত: আয়াত: ৩৭।

[11] ১০] সূরা আল-আরাফ: আয়াত :৫৪।

Arshi yake. Huufunika usiku kwa mchana, huufuatisha upesi upesi, Na ameliumba Jua na Mwezi

na nyota na vyote vimetiishwa kwa amri yake Mwenyezi Mungu, Fahamuni kuumba ni kwakwe tu mwenyewe (Mwenyezi Mungu) na amri zote ni zake (Mwenyezi Mungu) ametukuka Mwenyezi Mungu Mola wa walimwengu wote". Suratul A'raf Aya ya: 54.

Na Mola ndiye muabudiwa, na ushahidi ni kauli yake Mtukufu:

﴿يَٰٓأَيُّهَا ٱلنَّاسُ ٱعۡبُدُواْ رَبَّكُمُ ٱلَّذِي خَلَقَكُمۡ وَٱلَّذِينَ مِن قَبۡلِكُمۡ لَعَلَّكُمۡ تَتَّقُونَ ٢١ ٱلَّذِي جَعَلَ لَكُمُ ٱلۡأَرۡضَ فِرَٰشٗا وَٱلسَّمَآءَ بِنَآءٗ وَأَنزَلَ مِنَ ٱلسَّمَآءِ مَآءٗ فَأَخۡرَجَ بِهِۦ مِنَ ٱلثَّمَرَٰتِ رِزۡقٗا لَّكُمۡۖ فَلَا تَجۡعَلُواْ لِلَّهِ أَندَادٗا وَأَنتُمۡ تَعۡلَمُونَ ٢٢﴾[البقرة: 21-22].[12]

"Enyi watu! Muabuduni Mwenyezi Mungu Ambaye Amekuumbeni nyinyi, na akawaumba waliokuwa kabla yenu ili mpate kumcha Mwenyezi Mungu". "Mola wenu ni Yule Aliyewafanyia Ardhi iwe ni Tandiko, ili maisha yenu yawe mepesi juu yake, na

Mbingu ziwe zimejengeka madhubuti, na Akateremsha mvua kutoka kwenye

mawingu, Akatoa kutokana na mvua hiyo Matunda na Mimea aina mbali mbali ili iwe ni riziki kwenu. Basi,

[12] ১১] সূরা আল-বাকারার দু'টি আয়াত: ২১-২২।

msimuwekee Mwenyezi Mungu washirika katika Ibada, hali nyinyi mnajua kuwa Mwenyezi Mungu Amepwekeka katika kuumba, kuruzuku na kustahiki kuabudiwa". Suratul Baqara: 21,22.

Amesema bin Kathir Mwenyezi Mungu Mtukufu amrehemu: Muumba wa vitu hivi ndiye anayestahiki kuabudiwa.

# Aina za Ibada alizoziamrisha Mwenyezi Mungu.

(Na aina za Ibada) alizoziamrisha Mwenyezi Mungu mfano kama Uislamu na Imani, na Wema, na miongoni mwazo ni Dua na Hofu na Kutaraji na Kutegemea kwa Allah na kuwa na Shauku, na Woga, na Unyenyekevu, na Kutubia, na Kutaka msaada, na Kuomba kinga, na Kuomba Mvua, na Kuchinja, na Kuweka Nadhiri, na mengineyo miongoni mwa Ibada alizoziamrisha Mwenyezi Mungu (zote hizo ni kwa ajili ya Mwenyezi Mungu), na

ushahidi ni kauli yakeMwenyezi Mungu Mtukufu:

﴿وَأَنَّ ٱلۡمَسَٰجِدَ لِلَّهِ فَلَا تَدۡعُواْ مَعَ ٱللَّهِ أَحَدٗا ١٨﴾[الجن: 18].[13]

"Na kwa hakika Misikiti ni ya kuabudiwa Mwenyezi Mungu Peke yake, basi msiabudu humo asiyekuwa yeye"[14]Suratul Jinn, Aya: 18.

Atakayekielekeza chochote miongoni mwa Ibada hizo kwa asiyekuwa Mwenyezi Mungu basi huyo ni Mshirikina, na ushahidi ni kauli yake Mtukufu:

---

[13] ১২] সূরা আল-জিন: আয়াত:১৮।

[14] Suratul Jinn, Aya: 18.

﴿وَمَن يَدۡعُ مَعَ ٱللَّهِ إِلَٰهًا ءَاخَرَ لَا بُرۡهَٰنَ لَهُۥ بِهِۦ فَإِنَّمَا حِسَابُهُۥ عِندَ رَبِّهِۦٓۚ إِنَّهُۥ لَا يُفۡلِحُ ٱلۡكَٰفِرُونَ ١١٧﴾[المؤمنون: 117][15]

"Na yeyote atakayeabudu, pamoja na Mwenyezi Mungu Aliyepwekeka, Mungu mwingine, hana hoja yoyote juu ya ustahiki wake wa kuabudiwa. Basi kwa kweli malipo

yake juu ya kitendo chake hicho kiovu yako mbele ya Mola wake huko Akhera. Ukweli ni

kwamba hakuna kufuzu wala kuokoka kwa Makafiri Siku ya Kiyama". Suratul Muuminuun: 117.

Na imekuja katika Hadithi: (Dua ni ubongo wa ibada)[16], Na ushahidi ni kauli yakeMwenyezi Mungu Mtukufu: "Na Amesema Mola wenu,

﴿وَقَالَ رَبُّكُمُ ٱدۡعُونِيٓ أَسۡتَجِبۡ لَكُمۡۚ إِنَّ ٱلَّذِينَ يَسۡتَكۡبِرُونَ عَنۡ عِبَادَتِي سَيَدۡخُلُونَ جَهَنَّمَ دَاخِرِينَ ٦٠﴾[غافر: 60][17]

«Enyi waja! Niombeni peke yangu, nikukubalieni maombi yenu. Hakika ya wale wenye kufanya Kiburi kwa kukataa kunipwekesha katika Ibada na ustahiki wa

---

15 ১৩] সূরা আল-মু'মিনূন, আয়াত: ১১৭।
16 Kaipokea Tirmidhiy mlango da'waat (3371).
17 ১৪] তিরমিযী, দু'আসমূহ (অধ্যায়): ৩৩৭১।

kuabudiwa wataingia Moto wa Jahanamu wakiwa madhalili na wanyonge". Suratu Ghaafir: 60.[18]

Na ushahidi wakuwa na hofu, ni kauli yake Mwenyezi Mtukufu:

﴿... فَلَا تَخَافُوهُمۡ وَخَافُونِ إِن كُنتُم مُّؤۡمِنِينَ ١٧٥﴾[آل عمران: 175][19]

"Msiwaogope, niogopeni mimi ikiwa nyinyi ni waumini wa kweli"[20]Surat Al Imran: 175

Na ushahidi wa kutaraji, ni kauli yake Mtukufu:

﴿.... فَمَن كَانَ يَرۡجُواْ لِقَآءَ رَبِّهِۦ فَلۡيَعۡمَلۡ عَمَلٗا صَٰلِحٗا وَلَا يُشۡرِكۡ بِعِبَادَةِ رَبِّهِۦٓ أَحَدَۢا ١١٠﴾[الكهف: 110][21]

"Basi yeyote anayetaraji kukutana na Mola wake, basi na afanye matendo mema, na wala asimshirikishe katika ibada ya Mola wake yeyote"[22]Suratul Al Kahfi:110

Na ushahidi wa kutegemea kwa Allah, ni kauli yake Mtukufu:

---

[18] Suratu Ghaafir: 60.
[19] ১৬] সূরা আলে ইমরান: আয়াত : ১৭৫।
[20] . Surat Al Imran: 175
[21] ১৭] সূরা আল-কাহফ, আয়াত: ১১০।
[22] . Al Kahfi: 110.

﴿... وَعَلَى ٱللَّهِ فَتَوَكَّلُوٓاْ إِن كُنتُم مُّؤۡمِنِينَ ٢٣﴾[المائدة: 23][23]

{Na juu ya Mwenyezi Mungu basi tegemeeni ikiwa nyinyi ni Waumini kweli}. [Suratul Maidah: Aya ya 23]

﴿... وَمَن يَتَوَكَّلۡ عَلَى ٱللَّهِ فَهُوَ حَسۡبُهُۥٓ...﴾[الطلاق: 3][24]

"Na mwenye kumtegemea Mwenyezi Mungu basi yeye humtosheleza"[25]. Suratu Twalaq: 3.[26]

Na ushahidi wa kuwa na shauku na hofu na unyenyekevu, ni kauli yake Mtukufu: "Hakika wao walikuwa wakienda mbio katika mambo ya kheri, na wakituomba sisi kwa shauku (ya kuyapata yale mazuri waliyoahidiwa) na hofu (ya kuogopa wasipatwe na mabaya ya adhabu walizo tahadharishwa) na walikuwa kwetu sisi ni wanyenyekevu".

Na ushahidi wakuwa na woga, ni kauli yakeMwenyezi Mungu Mtukufu:

---

[23] ১৮] সূরা আল-মায়েদা: ২৩।

[24] ১৯] সূরা আত্ব-ত্বলাক, আয়াত: ৩।

[25] . Maida, Aya 23.

[26] . Suratu Twalaq: 3.

﴿... فَلَا تَخۡشَوۡهُمۡ وَٱخۡشَوۡنِۚ...﴾[المائدة: 3][27]

"Msiwaogope na niogopeni mimi"[28]Mpaka mwisho wa Aya, Suratul Maidah: Aya ya 3.

Na ushahidi wa kutubia ni kauli yakeMwenyezi Mungu Mtukufu:

﴿وَأَنِيبُوٓاْ إِلَىٰ رَبِّكُمۡ وَأَسۡلِمُواْ لَهُۥ...﴾[الزمر: 54][29]

"Na tubieni kwa Mola wenu na mjisalimishe kwake"[30]Mpaka mwisho wa Aya, suratu Al zzumar Aya ya: 54.

Na ushahidi wa kuomba msaada, ni kauli yake Mtukufu:

﴿إِيَّاكَ نَعۡبُدُ وَإِيَّاكَ نَسۡتَعِينُ٥﴾[الفاتحة: 5][31]

"Wewe tu ndiye tunayekuabudu na wewe tu ndiye tunayekuomba msaada".[32]Al Faatiha: Aya ya 5

Na imekuja katika Hadithi:

---

[27] ২১] সূরা আল-বাকারাহ, আয়াত: ১৫০।

[28] . Al Baqara: Aya ya: 150.

[29] ২২] সূরা আয-যুমার, আয়াত: ৫৪।

[30] . Al zzumar: 54.

[31] ২৩] সূরা আল-ফাতিহা, আয়াত: ০৫।

[32] Suratul Faatiha Aya: 5.

﴿قُلۡ أَعُوذُ بِرَبِّ ٱلنَّاسِ ١ مَلِكِ ٱلنَّاسِ ٢﴾[الناس: 1-2][33]

"Utakapotaka msaada basi taka msaada kwa Mwenyezi Mungu"[34].

Na ushahidi wa kuomba kinga, ni kauli yake Mwenyezi MunguMtukufu: "Sema, Ewe Mtume, «Ninajilinda na kutaka hifadhi kwa Bwana wa watu" "Mfalme wa watu" (2)[35]

Na ushahidi wa kuomba mvua, ni kauli yake Mtukufu:

﴿إِذۡ تَسۡتَغِيثُونَ رَبَّكُمۡ فَٱسۡتَجَابَ....﴾[الأنفال: 9][36]

"Pindi mlipomtaka msaada wa Mvua Mola wenu akakujibuni"[37]Mpaka mwisho wa Aya, Al Anfal Aya ya 9.

Na ushahidi wa kuchinja, ni kauli yake Mtukufu: Sema, ewe Mtume, kuwaambia

hawa washirikina, «Hakika Swala yangu na Nusuk yangu, yaani kuchinja kwangu ni kwa ajili ya Mwenyezi

---

33 ২৫] সূরা আন-নাস, আয়াত: ১-২।
34 Kaipokea Attirmidhy Swifatul Qiyama warraqaaiq wala waraa (2516), Ahmad (1/308).
35 Suratu Nnas Aya mbili: 1-2.
36 ২৬] সূরা আল-আনফাল, আয়াত: ০৯।
37 Suratu Al Anfal Aya ya 9.

Mungu, Peke yake; Pia uhai wangu na kufa kwangu ni kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, Mola wa viumbe wote".

﴿قُلْ إِنَّ صَلَاتِي وَنُسُكِي وَمَحْيَايَ وَمَمَاتِي لِلَّهِ رَبِّ ٱلْعَٰلَمِينَ ﴿١٦٢﴾ لَا شَرِيكَ لَهُۥ وَبِذَٰلِكَ أُمِرْتُ وَأَنَا۠ أَوَّلُ ٱلْمُسْلِمِينَ ﴿١٦٣﴾﴾[الأنعام: 162-163][38]

«Asiye na mshirika katika Uungu wake wala katika Umiliki wake wala katika majina yake na sifa zake. Kumpwekesha huko Mwenyezi Mungu kulikosafishika ndiko Alikoniamrisha mimi Mola wangu, Aliyetukuka na kuwa juu. Na mimi ni wa kwanza kumfuata Mwenyezi Mungu kikamilifu katika Umma huu.» (163)[39]Suratul An a'am 162, 163.

Na katika mafundisho ya Mtume Rehema na Amani ziwe juu yake: "Amemlaani

Mwenyezi Mungu mwenye kuchinja kwa ajili ya asiyekuwa Mwenyezi Mungu"[40].

Na ushahidi wa kuweka Nadhiri ni kauli yakeMwenyezi Mungu Mtukufu:

---

[38] ২৭] সূরা আল-আন‘আম, আয়াত: ১৬২-১৬৩।

[39] Suratul An a'am: Aya 162-163.

[40] Akipokea Muslim mlango wa Adhwaahi (1978), na Nasaai Mlango wa Dhwahaayaa (4422), Ahmad (1/118).

﴿يُوفُونَ بِٱلنَّذۡرِ وَيَخَافُونَ يَوۡمٗا كَانَ شَرُّهُۥ مُسۡتَطِيرٗا ٧﴾[الإنسان: 7].[41]

"Hao walikuwa huko duniani wanatekeleza kile walichojilazimisha nafsi zao cha utiifu kwa Mwenyezi Mungu, na wakiogopa mateso ya Mwenyezi Mungu, Siku ya Kiyama, ambayo madhara yake ni hatari na ubaya ni wenye kusambaa na kuenea kwa watu isipokuwa wale ambao Mwenyezi Mungu amewarehemu." Suratu Dahar: Aya ya 7.

Mwenyezi Mungu mwenye kuchinja kwa ajili ya asiyekuwa Mwenyezi Mungu"[42].

---

[41] ২৯] সূরা আল-ইনসান, আয়াত:৭।

[42] Akipokea Muslim mlango wa Adhwaahi (1978), na Nasaai Mlango wa Dhwahaayaa (4422), Ahmad (1/118).

## Msingi wa pili: Ni kuijua dini ya Uislamu kwa ushahidi.

Nako ni kujisalimisha kwa Mwenyezi Mungu kwa kumpwekesha, na kunyenyekea kwa utiifu, na kujiepusha na ushirikina. Nazo ni daraja tatu:

(Uislamu) na (Imani) Na (Ihsani), na kila Daraja lina nguzo zake.

### Daraja la Kwanza ni Uislamu:

Nguzo za Uislamu ni (tano) Kushuhudia kuwa hapana Mola apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Mwenyezi Mungu, na kuwa Muhammadi ni Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, na (Kusimamisha swala) na (Kutoa Zaka) na (kufunga Ramadhani) na (Kuhiji nyumba tukufu ya Mwenyezi Mungu).

Basi ushahidi wa shahada (kushuhudia kuwa hapana Mola apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Mwenyezi Mungu) ni kauli yake Mungu Mtukufu:

﴿شَهِدَ ٱللَّهُ أَنَّهُۥ لَآ إِلَٰهَ إِلَّا هُوَ وَٱلۡمَلَٰٓئِكَةُ وَأُوْلُواْ ٱلۡعِلۡمِ قَآئِمَۢا بِٱلۡقِسۡطِۚ لَآ إِلَٰهَ إِلَّا هُوَ ٱلۡعَزِيزُ ٱلۡحَكِيمُ ١٨﴾ [آل عمران: 18].[43]

"Mwenyezi Mungu ameshuhudia kuwa yeye ndiye aliyepwekeka kwa uungu. Na ameambatanisha ushahidi wake na ule wa Malaika na watu wa elimu juu ya kitu kitukufu zaidi chenye kushuhudiwa, nacho ni Tawhīid umoja wake aliyetukuka na kusimamia kwake haki na uadilifu. Hapana Mola isipokuwa yeye, aliye mshindi ambaye hakuna kitu atakacho kiwe kikakataa kuwa, Mwenye hekima katika maneno yake na vitendo vyake". Surat Al Imran: 18

, Na maana yake: Hakuna apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Mwenyezi Mungu pekee, Na neno (Laa ilaaha - Hapana Mola) Linakanusha yote yenye kuabudiwa kinyume na Mwenyezi Mungu, (illallaah -Isipokuwa Mwenyezi Mungu) Hili linathibitisha kuwa ibada ni za Mwenyezi Mungu peke yake asiyekuwa na mshirika katika Ibada zake, kama ambavyo hana mshirika wake katika Ufalme wake. Na

Tafsiri yake inawekwa wazi na kauli yake Mtukufu:

43 ৩০] সূরা আলে ইমরান: আয়াত : ১৮।

﴿وَإِذۡ قَالَ إِبۡرَٰهِيمُ لِأَبِيهِ وَقَوۡمِهِۦٓ إِنَّنِي بَرَآءٞ مِّمَّا تَعۡبُدُونَ ٢٦ إِلَّا ٱلَّذِي فَطَرَنِي فَإِنَّهُۥ سَيَهۡدِينِ ٢٧ وَجَعَلَهَا كَلِمَةَۢ بَاقِيَةٗ فِي عَقِبِهِۦ لَعَلَّهُمۡ يَرۡجِعُونَ ٢٨﴾[الزخرف: 26-28].[44]

"Kumbuka, ewe Mtume, pindi aliposema Ibrāhīm kumwambia Baba yake na watu wake waliokuwa wakiabudu vitu ambavyo watu wako ewe Mtume, wanaviabudu, ”Hakika mimi nimejiepusha na vile mnavyoviabudu badala ya Mwenyezi Mungu." «Isipokuwa yule aliyeniumba , kwani yeye ataniafikia kufuata njia ya uongofu.” Na Ibrāhīm, amani imshukie, alilifanya neno la kumpwekesha Mwenyezi Mungu (Lā ilāha illā Allāh) ni lenye kusalia baada yake, kwa kutarajiwa warudi kumtii Mola wao na kumpwekesha. Na kutubia kutokana na ukanushaji wao na dhambi zao"[45]. Zukhruf Aya ya: 26-27-28.[46]

Na kauli yake Mtukufu:

---

44 ৩১] সূরা আয-যুখরুফ, আয়াত: ২৬-২৮।

45 . Al Imran: 18

46 Suratu Zukhruf Aya ya: 26-27-28.

﴿قُلۡ يَٰٓأَهۡلَ ٱلۡكِتَٰبِ تَعَالَوۡاْ إِلَىٰ كَلِمَةٖ سَوَآءِۭ بَيۡنَنَا وَبَيۡنَكُمۡ أَلَّا نَعۡبُدَ إِلَّا ٱللَّهَ وَلَا نُشۡرِكَ بِهِۦ شَيۡـٔٗا وَلَا يَتَّخِذَ بَعۡضُنَا بَعۡضًا أَرۡبَابٗا مِّن دُونِ ٱللَّهِۚ فَإِن تَوَلَّوۡاْ فَقُولُواْ ٱشۡهَدُواْ بِأَنَّا مُسۡلِمُونَ ٦٤﴾[آل عمران: 64].[47]

"Sema, ewe Mtume, kuwaambia watu wa Kitabu miongoni mwa Mayahudi na Wanaswara, «Njooni kwenye neno la uadilifu na haki tushikamane nalo sote. Nalo ni sisi kuielekeza Ibada yetu kwa Mwenyezi Mungu peke yake. Na tusimfanye yeyote kuwa ni mshirika pamoja na yeye, awe ni Sanamu au Msalaba au Shetani au kinginecho. Na wala wasiwafanye baadhi yetu watu wengine kuwa ni Miungu badala ya Mwenyezi Mungu.» Basi wakiukataa wito huu mzuri, waambieni wao, enyi Waumini, «Kuweni ni mashahidi kwetu kuwa sisi tumejisalimisha kwa Mola wetu na tumenyoosha shingo zetu Kwake kwa kukubali kuwa ni waja wake na kwa kumtakasa.» Na wito huu kwenye neno la

sawa, kama unavyoelekezwa kwa Mayahudi na Wanaswara, unaelekezwa pia kwa wenye mwenendo kama wao". Surat Al Imran: 64

Na ushahidi wa kushuhudia kuwa Muhammadi ni Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ni kauli yake Mtukufu:

[47] ৩২] সূরা আলে ইমরান: আয়াত : ৬৪।

﴿لَقَدۡ جَآءَكُمۡ رَسُولٞ مِّنۡ أَنفُسِكُمۡ عَزِيزٌ عَلَيۡهِ مَا عَنِتُّمۡ حَرِيصٌ عَلَيۡكُم بِٱلۡمُؤۡمِنِينَ رَءُوفٞ رَّحِيمٞ ١٢٨﴾[التوبة: 128].[48]

"Hakika amewajia nyinyi, enyi Waumini, Mjumbe atokanaye na watu wenu, Azionea uzito shida mlizonazo na Tabu, ana pupa kwamba muamini na mambo yenu yafaulu na yeye kwa Waumini ni mwingi wa upole na huruma"[49]. Attaubah: 128

. Na maana ya Shahada ya kwamba "Muhammad ni Mjumbe wa Mwenyezi Mungu": Ni kumtii Mtume katika yale aliyo yaamrisha, na kumsadikisha katika yale aliyo yaeleza, na kujiepusha na yale aliyo yakataza na

kuyakemea, na asiabudiwe Mwenyezi Mungu isipokuwa kwa namna alivyo elekeza,

Na ushahidi wa swala na zaka na tafsiri ya tauhidi ni kauli yake Mtukufu:

[48] ৩৩] সূরা আত-তাওবাহ, আয়াত: ১২৮।

[49] Al Tauba: Aya:1287.

﴿وَمَآ أُمِرُوٓاْ إِلَّا لِيَعۡبُدُواْ ٱللَّهَ مُخۡلِصِينَ لَهُ ٱلدِّينَ حُنَفَآءَ وَيُقِيمُواْ ٱلصَّلَوٰةَ وَيُؤۡتُواْ ٱلزَّكَوٰةَۚ وَذَٰلِكَ دِينُ ٱلۡقَيِّمَةِ ٥﴾[البينة: 5][50]

"Na hawakuamrishwa katika sheria zote zilizopita isipokuwa wamuabudu Mwenyezi Mungu peke yake, wakikusudia kwa ibada yao kupata Radhi zake, hali ya kuepuka upande wa ushirikina na kuelekea kwenye Imani, wasimamishe Swala na watoe Zaka. Kufanya hayo ndio Dini iliyolingana, nayo ni Uislamu"[51]. Al Bayyina: Aya ya 5

Na ushahidi wa Swaumu, ni kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu:

﴿يَـٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ كُتِبَ عَلَيۡكُمُ ٱلصِّيَامُ كَمَا كُتِبَ عَلَى ٱلَّذِينَ مِن قَبۡلِكُمۡ لَعَلَّكُمۡ تَتَّقُونَ ١٨٣﴾[البقرة: 183][52]

"Enyi ambao mmemuamini Mwenyezi Mungu na Mtume wake na mkaifuata Sheria yake kivitendo, Mwenyezi Mungu Amewafaradhishia kufunga, kama Alivyowafaradhishia umma waliokuweko kabla yenu, ili mpate kumcha Mola wenu na kuweka kinga kati yenu na maasia, kwa kumtii na kumuabudu peke yake"[53]. Surat-Al-baqara Aya ya:183.

---

50 ৩৪] সূরা আল-বাইয়িনাহ, আয়াত: ৫।

51 . Al Bayyina: 5.

52 ৩৫] সূরা আল-বাকারা, আয়াত: ১৮৩।

53 . Al Baqara: Aya ya: 183.

Na ushahidi wa kuhiji, ni kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu:

﴿فِيهِ ءَايَٰتُۢ بَيِّنَٰتٞ مَّقَامُ إِبۡرَٰهِيمَۖ وَمَن دَخَلَهُۥ كَانَ ءَامِنٗاۗ وَلِلَّهِ عَلَى ٱلنَّاسِ حِجُّ ٱلۡبَيۡتِ مَنِ ٱسۡتَطَاعَ إِلَيۡهِ سَبِيلٗاۚ وَمَن كَفَرَ فَإِنَّ ٱللَّهَ غَنِيٌّ عَنِ ٱلۡعَٰلَمِينَ ٩٧﴾[آل عمران: 97][54]

{Na Mwenyezi Mungu amewawajibishia watu wafanye Hijja katika nyumba hiyo, yule awezaye kufunga safari kwenda huko, na

atakayekanusha (Na asiende na haliyakuwa anauwezo) Basi Mwenyezi Mungu si muhitaji wa kuwahitajia walimwengu}[55]. Surat Al Imran: 97

## Daraja la pili: Imani.

Nayo iko zaidi ya sehemu sabini ya juu yake zaidi ni kauli ya (Laa ilaaha illa llaahu) Hapana Mola apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Mwenyezi Mungu, na ya chini yake zaidi ni kuondoa maudhi njiani, na kuwa na Haya (aibu) ni sehemu katika imani.

Na Nguzo zake ni Sita: Ni kumuamini Mwenyezi Mungu, na Malaika wake, na vitabu vyake, na Mitume wake, na Siku ya mwisho, na kuamini Qadari kheri yake na shari yake.

---

[54] ৩৬] সূরা আলে ইমরান: আয়াত : ৯৭।

[55] . Surat Al Imran: 97

Na ushahidi juu ya nguzo hizi sita ni kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu:

﴿۞ لَّيْسَ ٱلْبِرَّ أَن تُوَلُّوا۟ وُجُوهَكُمْ قِبَلَ ٱلْمَشْرِقِ وَٱلْمَغْرِبِ وَلَـٰكِنَّ ٱلْبِرَّ مَنْ ءَامَنَ بِٱللَّهِ وَٱلْيَوْمِ ٱلْـَٔاخِرِ وَٱلْمَلَـٰٓئِكَةِ وَٱلْكِتَـٰبِ وَٱلنَّبِيِّـۧنَ....﴾[البقرة: 177].[56]

"Hapana kheri, mbele ya Mwenyezi Mungu aliyetukuka,kwa kuelekea kwenye Swala upande wa mashariki na magharibi, iwapo hilo halitokamani na amri ya Mwenyezi Mungu na sheria yake. Hakika kheri yote iko katika imani ya aliyemuamini Mwenyezi Mungu na akamkubali kuwa ndiye muabudiwa, peke yake, Hana mshirika wake, na akaiamini Siku ya kufufuliwa na Malipo, na akawaamini Malaika wote na vitabu vyote vilivyoteremshwa, na Mitume wote bila kubagua"[57]Mpaka mwisho wa Aya. Surat- Al-Baqara Aya ya:177.

Na ushahidi wa Qadari (Makadirio ya Mwenyezi Mungu), ni kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu:

﴿إِنَّا كُلَّ شَىْءٍ خَلَقْنَـٰهُ بِقَدَرٍ ﴿٤٩﴾﴾[القمر: 49][58]

{Kwa hakika sisi tumekiumba kila kitu kwa kipimo}[59], Al Qamari: 49.

---

56 ৩৭] সূরা আল-বাকারাহ, আয়াত: ১৭৭।

57 . Al Baqara: Aya ya: 177.

58 ৩৮] সূরা আল-কামার, আয়াত: ৪৯।

## Daraja La Tatu Ni Ihsani: Ihsani ina nguzo moja:

Nayo ni kumuabudu Mwenyezi Mungu kana kwamba unamuona na ikiwa humuoni basi yeye anakuona, na ushahidi ni kauli yake Mtukufu:

﴿إِنَّ ٱللَّهَ مَعَ ٱلَّذِينَ ٱتَّقَواْ وَّٱلَّذِينَ هُم مُّحۡسِنُونَ ١٢٨﴾[النحل: 128][60]

Kwa hakika Mwenyezi Mungu, kutakata na sifa za upungufu ni kwake na kutukuka ni kwake, kwa taufiki yake, msaada wake, upaji nguvu wake na nusura yake yuko pamoja na waliomcha kwa kuyafuata aliyoyaamrisha na kuyaepuka

aliyoyakataza; na yuko pamoja na wale wanaotenda wema,"[61]. Al Nahli: 128.

Na kauli yake Mtukufu:

﴿وَتَوَكَّلۡ عَلَى ٱلۡعَزِيزِ ٱلرَّحِيمِ ٢١٧ ٱلَّذِي يَرَىٰكَ حِينَ تَقُومُ ٢١٨ وَتَقَلُّبَكَ فِي ٱلسَّٰجِدِينَ ٢١٩ إِنَّهُۥ هُوَ ٱلسَّمِيعُ ٱلۡعَلِيمُ ٢٢٠﴾[الشعراء: 217-220][62]

"Na umuachie jambo lako Mwenyezi Mungu, aliye mshindi ambaye hakuna wa kushindana naye wala wa kumlazimisha, Mwenye kurehemu ambaye hawaachi

---

59 . Al Qamari: Aya ya: 49.

60 ৩৯] সূরা আন-নাহল, আয়াত: ১২৮।

61 . (Al Nahli: 128).

62 ৪০] সূরা শু'আরা, আয়াত: ২১৭-২২০।

wenye kumtegemea" (217) "Ambaye anakuona unaposimama kuswali ukiwa peke yako ndani ya usiku" (218) "Na anaona vile unavyogeuka, pamoja na wenye kumsujudia katika Swala zao wakiwa na wewe, ukiwa katika hali ya kusimama, kurukuu na kusujudu na kuketi" (219). "Hakika yeye, kutakasika na sifa za upungufu ni kwake, ndiye anayesikia kusoma kwako na kumtaja kwako, ndiye

anayejua nia yako na matendo yako"[63]. Ash shu'raa: Aya ya 217-220.

Na kauli yake Mtukufu:

﴿وَمَا تَكُونُ فِي شَأْنٍ وَمَا تَتْلُواْ مِنْهُ مِن قُرْءَانٍ وَلَا تَعْمَلُونَ مِنْ عَمَلٍ إِلَّا كُنَّا عَلَيْكُمْ شُهُودًا...﴾[يونس: 61][64]

"Na huwi, ewe Mtume, kwenye jambo lolote katika mambo yako, na husomi chochote kile katika Aya za Kitabu cha Mwenyezi Mungu, na hafanyi yeyote katika umma huu tendo lolote jema au baya, isipokuwa sisi huwa ni mashahidi juu yenu ni wenye kuliona hilo, mnapolichukua na kulitenda, tukawahifadhia na tukawalipa kwalo"[65]. Yunus Aya ya: 61.

---

[63] Surat Ash shu'raa: Aya ya 217-220.
[64] ৪১] সূরা ইউনুস, আয়াত: ৬১।
[65] . Suratu Yunus: 161.

(Na ushahidi kutoka katika maneno ya Mtume): Ni Hadithi Mashuhuri ya Jibrili kutoka kwa Omari bin Khattwab -Radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake- Amesema:

"Tukiwa sisi tumekaa kwa Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- siku moja, ghafla akatokeza mwanaume mmoja, mwenye nguo nyeupe sana, mwenye nywele nyeusi

sana, hazionekani kwake athari za Safari, na wala hakuna anayemfahamu yeyote katika sisi, mpaka akakaa kwa Mtume Rehema na Amani ziwe juu yake akashikanisha Magoti yake katika Magoti ya Mtume Rehema na Amani ziwe juu yake (mfano wa kikao cha Tahiyatu) na akaweka Mikono yake juu ya Mapaja yake, Na akasema: Ewe Muhammadi, nieleze kuhusu Uislamu? Akasema Mjumbe wa Mwenyezi Mungu Rehema na Amani ziwe juu yake: Uislamu ni kushuhudia kuwa hapana Mola apasaye kuabudiwa isipokuwa Mwenyezi Mungu nakuwa Muhammadi ni Mtume wa Mwenyezi Mungu, na usimamishe swala na utoe zaka, na ufunge Ramadhani, na Uhiji nyumba tukufu ukipata uwezo wa kuifikia, Yule Bwana akasema: "Swadakta"-Yaani: Umesema kweli, Tukamshangaa! Anamuuliza na anamsadikisha!.

Akasema: Nieleze kuhusu Imani? Akasema: Ni kumuamini Mwenyezi Mungu na Malaika

wake na vitabu vyake na Mitume wake na siku ya mwisho, na uamini makadirio kheri yake na shari yake, Akasema: "Swadakta"-

Yaani: Umesema kweli, Basi hebu nieleze kuhusu Ihsani (wema)? Akasema: Ni umuabudu Mwenyezi Mungu kana kwamba wewe unamuona, na ikiwa wewe humuoni basi yeye anakuona: Akasema: Hebu nieleze kuhusu kiyama: Akasema: hakuwa muulizwaji kuhusu hilo ni mjuzi kuliko muulizaji, Akasema: Hebu nieleze kuhusu dalili zake? akashikanisha Magoti yake katika Magoti ya Mtume Rehema na Amani ziwe juu yake (mfano wa kikao cha Tahiyatu) na akaweka Mikono yake juu ya Mapaja yake, Na akasema: Ewe Muhammadi, nieleze kuhusu Uislamu? Akasema Mjumbe wa Mwenyezi Mungu Rehema na Amani ziwe juu yake: Uislamu ni kushuhudia kuwa hapana Mola apasaye kuabudiwa isipokuwa Mwenyezi Mungu nakuwa Muhammadi ni Mtume wa Mwenyezi Mungu, na usimamishe swala na utoe zaka, na ufunge Ramadhani, na Uhiji nyumba tukufu ukipata uwezo wa kuifikia, Yule Bwana akasema: "Swadakta"-Yaani: Umesema kweli, Tukamshangaa! Anamuuliza na anamsadikisha!.

Akasema: Nieleze kuhusu Imani? Akasema: Ni kumuamini Mwenyezi Mungu na Malaika

Tahiyatu) na akaweka Mikono yake juu ya Mapaja yake, Na akasema: Ewe Muhammadi, nieleze kuhusu Uislamu? Akasema Mjumbe wa Mwenyezi Mungu Rehema na Amani ziwe juu yake: Uislamu ni kushuhudia kuwa hapana Mola apasaye kuabudiwa isipokuwa Mwenyezi Mungu nakuwa Muhammadi ni Mtume wa Mwenyezi Mungu, na usimamishe swala na utoe zaka, na ufunge Ramadhani, na Uhiji nyumba tukufu ukipata uwezo wa kuifikia, Yule Bwana akasema: "Swadakta"-Yaani: Umesema kweli, Tukamshangaa! Anamuuliza na anamsadikisha!.

Akasema: Nieleze kuhusu Imani? Akasema: Ni kumuamini Mwenyezi Mungu na Malaika

wake na vitabu vyake na Mitume wake na siku ya mwisho, na uamini makadirio kheri yake na shari yake, Akasema: "Swadakta"-

Yaani: Umesema kweli, Basi hebu nieleze kuhusu Ihsani (wema)? Akasema: Ni umuabudu Mwenyezi Mungu kana kwamba wewe unamuona, na ikiwa wewe humuoni basi yeye anakuona: Akasema: Hebu nieleze kuhusu kiyama: Akasema: hakuwa muulizwaji kuhusu hilo ni mjuzi kuliko muulizaji, Akasema: Hebu

## Msingi wa tatu: Ni kumjua Nabii wenu Muhammad - Rehema za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake na amani-

Naye ni Muhammadi bin Abdillah bin Abil Muttwalib bin Hashim, Na Hashim ni katika Makuraishi, na Makuraishi ni katika

Waarabu, na Waarabu wanatokana na kizazi cha Ismaili bin Ibrahim kipenzi wa Mwenyezi Mungu kwake na kwa Nabii wetu Amani iwe juu yao.

Mtume wa Mwenyezi Mungu, na usimamishe swala na utoe zaka, na ufunge Ramadhani, na Uhiji nyumba tukufu ukipata uwezo wa kuifikia, Yule Bwana akasema: "Swadakta"-Yaani: Umesema kweli, Tukamshangaa! Anamuuliza na anamsadikisha!.

Akasema: Nieleze kuhusu Imani? Akasema: Ni kumuamini Mwenyezi Mungu na Malaika

wake na vitabu vyake na Mitume wake na siku ya mwisho, na uamini makadirio kheri yake na shari yake, Akasema: "Swadakta"-

Yaani: Umesema kweli, Basi hebu nieleze kuhusu Ihsani (wema)? Akasema: Ni umuabudu Mwenyezi Mungu kana kwamba wewe unamuona, na ikiwa wewe humuoni basi

yeye anakuona: Akasema: Hebu nieleze kuhusu kiyama: Akasema: hakuwa muulizwaji kuhusu hilo ni mjuzi kuliko muulizaji, Akasema: Hebu

Na alikuwa na umri wa miaka sitini na tatu (63) katika hiyo, miaka Arobaini (40) ilikuwa kabla ya utume, na miaka ishirini na tatu (23) akiwa Nabii na Mtume. Alipewa Unabii kwa neno (Iqraa) Yaani: Soma. Na akapewa Utume kwa neno (Muddathir) Yaani: Aliyejifunika. Mji wake ni Makka, Mwenyezi Mungu alimtuma ili kuwaonya watu na ushirikina, na awaite kuja katika kumpwekesha Mwenyezi Mungu (Tauhidi), na ushahidi ni kauli yake Mtukufu:

﴿يَـٰٓأَيُّهَا ٱلْمُدَّثِّرُ ۝١ قُمْ فَأَنذِرْ ۝٢ وَرَبَّكَ فَكَبِّرْ ۝٣ وَثِيَابَكَ فَطَهِّرْ ۝٤ وَٱلرُّجْزَ فَٱهْجُرْ ۝٥
وَلَا تَمْنُن تَسْتَكْثِرُ ۝٦ وَلِرَبِّكَ فَٱصْبِرْ ۝٧﴾[المدثر: 1-7][66]

"Ewe uliyejifunika nguo! (1) "Simama na uonye (2) "Na Mola wako umtukuze (3) "Na nguo zako uzisafishe" "Na mabaya yapuuze". Na usitoe kitu kumpa mtu kwa

lengo la kupata zaidi ya hicho. "Na kwa ajili ya Mola wako fanya Subira (7)[67]Al Muddathiri: 1-7.

[66] ৪৩] সূরা আল-মুদ্দাসসির, আয়াত: ১-৭।
[67] Surat Al Muddathiri: 1-7.

Na maana ya simama na uonye: Yaani aonye kutokana na ushirikina na awaite katika TauhIidi (kumpwekesha Mwenyezi Mungu, Na Mola wako umtukuze: Yaani mtukuze kwa Tauhidi, Na nguo zako zisafishe: Yaani: Safisha matendo yako kutokana na ushirikina, Na mabaya uyahame, Mabaya: Yaani Masanamu, na kuyahama kwake ni kuyaacha na kuwaacha wafanyaji wake, na kujiepusha nayo pamoja watu wake. Ametumia katika hili miaka kumi

akilingania katika Tauhidi, na baada ya miaka kumi alipandishwa kwenda mbinguni na zikafaradhishwa kwake swala Tano, na akaswali Makka miaka mitatu, na baada ya hapo akaamrishwa kuhamia Madina. Na kuhama: Ni kutoka katika mji wa kishirikina kwenda katika mji wa

﴿إِنَّ ٱلَّذِينَ تَوَفَّىٰهُمُ ٱلۡمَلَٰٓئِكَةُ ظَالِمِيٓ أَنفُسِهِمۡ قَالُواْ فِيمَ كُنتُمۡۖ قَالُواْ كُنَّا مُسۡتَضۡعَفِينَ فِي ٱلۡأَرۡضِۚ قَالُوٓاْ أَلَمۡ تَكُنۡ أَرۡضُ ٱللَّهِ وَٰسِعَةٗ فَتُهَاجِرُواْ فِيهَاۚ فَأُوْلَٰٓئِكَ مَأۡوَىٰهُمۡ جَهَنَّمُۖ وَسَآءَتۡ مَصِيرًا ٩٧ إِلَّا ٱلۡمُسۡتَضۡعَفِينَ مِنَ ٱلرِّجَالِ وَٱلنِّسَآءِ وَٱلۡوِلۡدَٰنِ لَا يَسۡتَطِيعُونَ حِيلَةٗ وَلَا يَهۡتَدُونَ سَبِيلٗا ٩٨ فَأُوْلَٰٓئِكَ عَسَى ٱللَّهُ أَن يَعۡفُوَ عَنۡهُمۡۚ وَكَانَ ٱللَّهُ عَفُوًّا غَفُورٗا ٩٩﴾[النساء: 97-99].[68]

. "Wanyonge hawa ndio wanaotarajiwa kupata msamaha kutoka kwa Mwenyezi Mungu aliyetukuka, kwa kuwa yeye anaujua uhakika wa mambo yao. Na Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa msamaha, Anawasamehe makosa yao na

Anawafunikia na kuwasitiria". (99)[69]An nisaai: 97-99.

Na kauli yake Mtukufu:

﴿يَٰعِبَادِيَ ٱلَّذِينَ ءَامَنُوٓاْ إِنَّ أَرۡضِي وَٰسِعَةٞ فَإِيَّٰيَ فَٱعۡبُدُونِ ٥٦﴾ [العنكبوت: 56].[70]

«Enyi waja wangu mlioamini! Iwapo mna shida ya kudhihirisha Imani na Ibada ya Mwenyezi Mungu peke yake, basi hamieni kwenye Ardhi ya Mwenyezi Mungu iliyo kunjufu na mnitakasie Ibada mimi peke yangu.» Al-ankabuut: Aya ya 56.

---

68 ৪৪] সূরা আন-নিসা, আয়াত: ৯৭-৯৯।

69 Suratu An nisaai: 97-99.

70 ৪৫] সূরা আল-আনকাবূত, আয়াত: ৫৬।

Na amesema Imamu Al Baghawiy, Allah amrehemu: Sababu ya kuteremka kwa Aya hii ni waislamu waliokuwa Makka hawakuhama, Mwenyezi Mungu akawaita kwa jina la imani. Na ushahidi unaoonyesha kuwa kuhama ni katika mafundisho ya Mtume ni kauli yake Rehema na Amani ziwe juu yake. "Hakutokatika kuhama mpaka ikatike Toba, na wala Toba haitokatika mpaka Jua lichomoze kutoka Magharibi

yake"[71]Alipoweka kituo katika mji wa Madina akaamrishwa sheria zingine za Uislamu zilizobakia kama Zaka, na

Swaumu, na Hija, na Adhana, na Jihadi, na kuamrisha mema na kukataza mabaya, na zinginezo katika sheria za uislamu, zimetumia muda huu wa miaka kumi.

Na alifariki Rehema na Amani ziwe juu yake na Dini yake ikabakia, na Dini yake hii, hakuna jambo zuri lolote isipokuwa aliujulisha Umma wake jambo hilo, wala jambo la shari isipokuwa aliutahadharisha Umma wake shari hiyo. Na Kheri aliyoujulisha umma wake kubwa zaidi ni Tauhidi (kumpwekesha Mwenyezi Mungu) na yote anayoyapenda Mwenyezi Mungu na kuyaridhia, na Shari

[71] Kaipokea Abuu Daud jihadi (2479), Na Ahmad (4/99), Na Daaramiy katika Assiyar (2513).

aliyoutahadharisha umma wake dhidi yake ni Ushirikina na yote anayoyachukia Mwenyezi Mungu na kuyakataa, Mwenyezi Mungu alimtuma kwa watu wote, na akawajibisha kumtii yeye kwa viumbe wawili waliopewa majukumu, yaani

Majini na Binadamu. Na ushahidi ni kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu:

﴿قُلۡ يَٰٓأَيُّهَا ٱلنَّاسُ إِنِّي رَسُولُ ٱللَّهِ إِلَيۡكُمۡ جَمِيعًا ...﴾[الأعراف: 158][72]

{Sema: Enyi watu! Hakika mimi ni Mtume kwenu nyinyi nyote}[73]. Al A'raaf: Aya 158

, Na Mwenyezi Mungu alikamilisha Dini kupitia yeye.

Na ushahidi ni kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu:

﴿...ٱلۡيَوۡمَ أَكۡمَلۡتُ لَكُمۡ دِينَكُمۡ وَأَتۡمَمۡتُ عَلَيۡكُمۡ نِعۡمَتِي وَرَضِيتُ لَكُمُ ٱلۡإِسۡلَٰمَ دِينٗاۚ ...﴾[المائدة: 3][74]

"Leo nimekukamilishieni Dini yenu na nimekutimizieni neema yangu, na nimekupendeleeni Uislamu uwe ndiyo Dini"[75]Suratul Maidah: Aya ya 3.

---

[72] ৪৭] সূরা আল-আ'রাফ: আয়াত :১৫৮।
[73] suratul A'raf Aya ya: 158.
[74] ৪৮] সূরা আল-মায়িদাহ, আয়াত: ৩।
[75] Maida, mpaka mwisho wa Aya 3.

Na ushahidi wa kifo chake -Rehema na Amani ziwe juu yake- ni kauli yake Mtukufu:

﴿إِنَّكَ مَيِّتٞ وَإِنَّهُم مَّيِّتُونَ ٣٠ ثُمَّ إِنَّكُمۡ يَوۡمَ ٱلۡقِيَٰمَةِ عِندَ رَبِّكُمۡ تَخۡتَصِمُونَ ٣١﴾[الزمر: 30-31].[76]

"Wewe ni mwenye kufa, ewe Mtume, na wao ni wenye kufa" (30) "Kisha nyote, Siku ya Kiyama. Kwa Mola wenu mtagombana"[77]Azzumar, 30,31

Na watu watakapokufa watafufuliwa, na ushahidi ni kauli yake Mtukufu:

﴿۞مِنۡهَا خَلَقۡنَٰكُمۡ وَفِيهَا نُعِيدُكُمۡ وَمِنۡهَا نُخۡرِجُكُمۡ تَارَةً أُخۡرَىٰ ٥٥﴾[طه: 55][78]

"Kutoka kwenye Ardhi tumewaumba na humo tutawarudisha tena baada ya kufa"[79]Twaha: 55

Na kauli yake Mtukufu:

---

[76] ৪৯] সূরা আয-যুমার, আয়াত: ৩০-৩১।

[77] Suratu zzumar: Aya mbili: 30, 31.

[78] ৫০] সূরা ত্বহা, আয়াত: ৫৫।

[79] Suratu Twaha: Aya ya 55.

﴿وَٱللَّهُ أَنۢبَتَكُم مِّنَ ٱلۡأَرۡضِ نَبَاتٗا ١٧ ثُمَّ يُعِيدُكُمۡ فِيهَا وَيُخۡرِجُكُمۡ إِخۡرَاجٗا ١٨﴾[نوح: 17-18].[80]

"Mwenyezi Mungu aliumba asili yenu kutokana na ardhi" (17) "kisha Atawarudisha humo Ardhini baada ya kufa, na Awatoe Siku ya kufufuliwa kuwatoa kihakika" (18)[81]. Nuhu: Aya ya: 17, 18 Na

baada ya kufufuliwa watahesabiwa na watalipwa kwa matendo yao, na ushahidi ni kauli yake Mtukufu:

﴿وَلِلَّهِ مَا فِي ٱلسَّمَٰوَٰتِ وَمَا فِي ٱلۡأَرۡضِ لِيَجۡزِيَ ٱلَّذِينَ أَسَٰٓـُٔواْ بِمَا عَمِلُواْ وَيَجۡزِيَ ٱلَّذِينَ أَحۡسَنُواْ بِٱلۡحُسۡنَى ٣١﴾[النجم: 31].[82]

"Ni ya Mwenyezi Mungu, aliyetakasika na kutukuka, mamlaka ya vilivyoko Mbinguni na vilivyoko Ardhini, ili awalipe wale waliokosa kwa kuwatesa kwa maovu waliyoyafanya na awalipe Pepo wale waliofanya wema"[83]. An Najmi Aya 31.

Na atakayepinga kufufuliwa atakuwa kakufuru, na ushahidi ni kauli yake Mtukufu:

---

80 ৫১] সূরা নূহ, আয়াত: ১৭-১৮।
81 Suratu Nuhu Aya mbili: 17-18.
82 ৫২] সূরা আন-নাজম, আয়াত: ৩১।
83 . An Najmu: 31.

﴿زَعَمَ ٱلَّذِينَ كَفَرُوٓاْ أَن لَّن يُبۡعَثُواْۚ قُلۡ بَلَىٰ وَرَبِّي لَتُبۡعَثُنَّ ثُمَّ لَتُنَبَّؤُنَّ بِمَا عَمِلۡتُمۡۚ وَذَٰلِكَ عَلَى ٱللَّهِ يَسِيرٞ ٧﴾[التغابن: 7].[84]

"Waliokufuru wanadai kuwa hawatofufuliwa, sema' kwa nini? kwa haki ya Mola wangu hakika nyinyi mtafufuliwa: kisha mtajulishwa mliyokuwa mnayatenda"[85]. Attaghaabun: Aya ya 7,

Na aliwatuma Mwenyezi Mungu Mitume wote ili watoe habari njema na wawaonye watu, na ushahidi ni kauli yakeMwenyezi Mungu Mtukufu:

﴿رُّسُلٗا مُّبَشِّرِينَ وَمُنذِرِينَ لِئَلَّا يَكُونَ لِلنَّاسِ عَلَى ٱللَّهِ حُجَّةُۢ بَعۡدَ ٱلرُّسُلِۚ وَكَانَ ٱللَّهُ عَزِيزًا حَكِيمٗا ١٦٥﴾[النساء: 165][86]

"Mitume hao ni Wabashiri na Waonyaji, ili watu wasiwe na hoja juu ya Mwenyezi

Mungu baada ya kuletewa Mitume"[87]An-nissa 165,

Na wa mwanzo wao ni Nuhu Amani ziwe juu yake na wa mwisho wao ni Muhammadi -Rehema na Amani ziwe juu yake, na yeye ndiye mwisho wa Manabii.

---

84 ৫৩] সূরা আত-তাগাবুন, আয়াত: ৭।

85 Suratu Taghaabun: 7.

86 ৫৪] সূরা আন-নিসা, আয়াত: ১৬৫।

87 . An Nisaa: Aya ya: 165.

Na ushahidi wa kuwa wa mwanzo wao ni Nuhu ni kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu:

﴿إِنَّآ أَوۡحَيۡنَآ إِلَيۡكَ كَمَآ أَوۡحَيۡنَآ إِلَىٰ نُوحٖ وَٱلنَّبِيِّـۧنَ مِنۢ بَعۡدِهِۦۚ...﴾ [النساء: 163].[88]

"Hakika sisi tumeteremsha wahyi kwako kama tulivyoteremsha wahyi kwa Nuhu na Manabii wengine baada yake"[89]An-nissa 163

, Na kila umma alioutumia Mwenyezi Mungu Mtume kwanzia kwa Nuhu mpaka kwa Muhammadi alikuwa akiwaamrisha kumuabudu Mwenyezi Mungu peke yake, na akiwakataza kumuabudu shetani, na ushahidi ni kauli yake Mtukufu:

﴿وَلَقَدۡ بَعَثۡنَا فِي كُلِّ أُمَّةٖ رَّسُولًا أَنِ ٱعۡبُدُواْ ٱللَّهَ وَٱجۡتَنِبُواْ ٱلطَّٰغُوتَۖ...﴾ [النحل: 36].[90]

{Na kwa hakika kwa kila umma tuliutumia Mtume kwamba: Muabuduni Mwenyezi Mungu, na muepukeni Shetani}[91]. An Nahli: 36

. Na akawawajibishia Mwenyezi Mungu waja wote kumkufuru Shetani na kumuamini Mwenyezi Mungu.

---

88 ৫৫] আন-নিসা, আয়াত: ১৬৩।

89 . An Nisaa: Aya ya: 163.

90 ৫৬] সূরা আন-নাহল, আয়াত: ৩৬।

91 . Al Nahli: 36.

Amesema Ibn Alqayim Allah Mtukufu amrehemu: Maana ya Twaghuti (shetani): Ni kila ambacho mja atavuka mpaka wake, kuanzia mwenye kuabudiwa au kufuatwa au kutiiwa, na Matwaghuti ni wengi. Na wakuu wao ni watano: Ibilisi Mwenyezi Mungu amlaani, na atakayeabudiwa naye akaridhia, na atakayewaita watu wamuabudu, na atakayedai kujua chochote katika elimu ya mambo yaliyofichikana, na atakayehukumu kinyume na yale aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu. Na ushahidi ni kauli yake Mtukufu: "Kwa kuwa Dini hii imekamilika na hoja zake ziko wazi,

haihitajii ilazimishwe kwa watu ambao jizia inapokewa kutoka kwao. Kwani dalili ziko wazi ambazo kwa dalili hizo inabainika haki, ikawa kando na batili, na uongofuAmesema Ibn Alqayim Allah Mtukufu amrehemu: Maana ya Twaghuti (shetani): Ni kila ambacho mja atavuka mpaka wake, kuanzia mwenye kuabudiwa au kufuatwa au kutiiwa, na Matwaghuti ni wengi. Na wakuu wao ni watano: Ibilisi Mwenyezi Mungu amlaani, na atakayeabudiwa naye akaridhia, na atakayewaita watu wamuabudu, na atakayedai kujua chochote katika elimu ya mambo yaliyofichikana, na atakayehukumu kinyume na yale aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu. Na ushahidi ni kauli yake Mtukufu, ukawa kando na upotevu. Basi mwenye kukanusha vyote vinavyoabudiwa badala ya

Mwenyezi Mungu na akamuamini Mwenyezi Mungu, huwa amethibiti na kulingana kwenye njia bora

﴿لَآ إِكۡرَاهَ فِي ٱلدِّينِۖ قَد تَّبَيَّنَ ٱلرُّشۡدُ مِنَ ٱلۡغَيِّۚ فَمَن يَكۡفُرۡ بِٱلطَّٰغُوتِ وَيُؤۡمِنۢ بِٱللَّهِ فَقَدِ ٱسۡتَمۡسَكَ بِٱلۡعُرۡوَةِ ٱلۡوُثۡقَىٰ لَا ٱنفِصَامَ لَهَاۗ وَٱللَّهُ سَمِيعٌ عَلِيمٌ ٢٥٦﴾[البقرة: 256].[92]

na ameshikamana na kamba imara ya Dini isiyokatika. Na Mwenyezi Mungu ni Msikivu wa maneno ya waja wake, ni Mjuzi wa nia zao na vitendo vyao na atawalipa kwa hayo"[93]. Surat- Al-baqara Aya ya: 256.

Na hii ndiyo maana ya Laa ilaaha illa llaah (Hapana Mola apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Mwenyezi Mungu).

---

[92] ৫৭] সূরা আল-বাক্বারাহ, আয়াত: ২৫৬।

[93] . Al Baqara: Aya ya: 256.

# . muhtasari

UTANGULIZI WA MSAMBAZAJI: ......................................................................4

MAMBO YA WAJIBU KWA MUISLAMU KUJIFUNZA: ....................................................7

UTAKASIFU AMBAO NI MILA YA IBRAHIM NDIYO IBADA YA KUMUABUDU MWENYEZI MUNGU PEKE YAKE. ......................................................................12

AINA ZA IBADA ALIZOZIAMRISHA MWENYEZI MUNGU. ................................................17

MSINGI WA PILI: NI KUIJUA DINI YA UISLAMU KWA USHAHIDI. ...................................25

MSINGI WA TATU: NI KUMJUA NABII WENU MUHAMMAD - REHEMA ZA MWENYEZI MUNGU ZIWE JUU YAKE NA AMANI-......................................................................38

. MUHTASARI ......................................................................50

ننشر الإسلام بأكثر من 100 لغة

موسوعة القرآن الكريم
QuranEnc.com
موسوعة تضم تفاسير وتراجم موثوقة لمعاني القرآن الكريم

موسوعة الأحاديث النبوية
HadeethEnc.com
موسوعة تضم ترجمات للأحاديث النبوية وشروحها بعدة لغات

موسوعة المصطلحات الإسلامية
TerminologyEnc.com
موسوعة تضم ترجمات المصطلحات الإسلامية وشروحها بعدة لغات

منتقى
موسوعة تضم المنتقى من المحتوى الإسلامي باللغات

IslamHouse.com
مرجعية مجانية الكترونية موثوقة للتعريف بالإسلام

جمعية الدعوة وتوعية الجاليات بالربوة

جمعية خدمة المحتوى الإسلامي باللغات